# Muhtasari wa Utafiti: Jiji la Dar es Salaam

AFRICAN CITIES RESEARCH CONSORTIUM

Soma ripoti kamili

**African Cities Research Consortium (ACRC) ni utafiti shirikishi unaoangalia namna ya kukabiliana na changamoto ngumu za maendeleo ya miji katika miji inayobadilika haraka barani. ACRC inalenga kuzalisha ufahamu thabiti na ushahidi ambao utasaidia kuboresha hali ya maisha na huduma za mijini kwa wakazi wote wa jiji, hasa jamii zisizojiweza.**

**Dar es Salaam (Dar) ni moja ya miji 12 ya Afrika ambapo ACRC inashirikisha mashirika ya kijamii, watafiti, watendaji, watendaji muhimu wa serikali na mashirika yasiyo ya serikali kushirikiana kuzalisha maarifa na ushahidi ili kuendeleza mabadiliko ya miji.**



## Matokeo muhimu

Jijini Dar es Salaam, utafiti wa ACRC ulijikita katika domains/maeneo manne ambavyo ni nyumba/makazi, makazi yasiyo rasmi (holela), mabadiliko ya kimuundo/mifumo na maendeleo ya kiuchumi katika jamii (kuanzia ujirani/kitongoji) na wilaya. Yaliyoangaziwa hapa chini ni matokeo muhimu kwa mabadiliko ya jiji.

> Wakazi wengi wa kipato cha chini jijini Dar es Salaam hawawezi kukidhi mahitaji yao ya nyumba na kupata fedha za makazi, badala yake kuchagua kujenga nyumba kwa kudunduliza, ambayo yanachangia ukuaji wa makazi yasiyo rasmi. Kuna haja ya kuonesha kwamba ujenzi wa nyumba za bei nafuu unaweza kuleta matokeo chanya katika kuleta makazi bora.

> Mikakati ya kuboresha makazi yasiyo rasmi hadi sasa haijazuia kuenea kwa makazi yasioyo rasmi. Mipango shirikishi inahitajika ili kuwaleta pamoja wadau na kuvutia fedha ili kusimamia kukua na kuenea kwa makazi yasiyo rasmi.

> Licha ya kuenea kwa ujenzi holela, kuna taratibu ngumu za kupata vibali vya ujenzi, ambazo zinachangia na kusababisha maendeleo ya jiji kuwa kiholela. Taratibu zisizoratibiwa vizuri kwa ajili ya maendeleo ya jiji kwenye ujenzi bado zinaendelea kuwepo. Itifaki za kutoa vibali vya ujenzi bado ni ngumu. Hivyo basi, ni vyema kukawa na center/sehemu moja kupitia huduma za mtandaoni ambapo utaratibu wa kupata vibali vya ujenzi utafanyika ili kuzuia kuenea kwa makazi holela.

> Pamoja na upatikanaji wa machaguo ya gharama nafuu, njia za uhakika za usafiri ni muhimu katika kukuza biashara katika ngazi za kawaida za jamii (kuanzia ujirani au kitongoji) na wilaya. Sekta ya pikipiki (bodaboda) inaziba pengo la usafiri lakini inakabiliwa na changamoto juu ya haja yakufanyika mageuzi/maboreshoili kuimarisha usalama wake.

# Muhtasari wa utafiti

## Mifumo ya mji

Dar es Salaam ilibadilika kupitia mipango mikuu mitatu yaani: villagisation, decentralization na mawazo ya "onna off" ya kuhamishia mji mkuu Dodoma. Nyayo za kihistoria za mipango hii zililenga mbali kwa kuangalia mji wa maendeleo yaliyokwama katika utoaji wa huduma za miundombinu.

Hivi sasa, utoaji wa huduma mbalimbali unaonesha uwepo wa sekta mbili yaani rasmi na isio rasmi, unaoendana na tofauti katika maendeleo ya miundombinu na hali ya kijamii na kiuchumi ya makazi. Mifumo rasmi inashikilia mifumo inayoonekana kuwa muhimu na nyeti kwa maendeleo ya rasilimali watu na usalama kama vile elimu, afya, sheria na taratibu. Licha ya sekta isiyo rasmi kutawala utoaji wa huduma kama vile maji taka na usafi wa mazingira, sehemu kubwa ya wakazi wa kipato cha chini wanapata kwa kiwango kisichostahili au bado hawapati huduma hizo.

Vikwazo vya rasilimali, wingi wa kanuni (sheria) na watendaji (wasimamiaji wengi), vikwazo vya kiutawala katika manispaa tano na uwepo wa nguvu kubwa ya kiutawala serikali kuu kunaathiri utendaji wa mifumo ya jiji iliyopo. Ingawa mifumo inategemeana na kuingiliana, haijaunganishwa vya kutosha, inapunguza ufanisi na ufasaha. Utendaji usiofaa wa mifumo unazuia ukuaji wa jumla wa jiji, mabadiliko/mageuzi na uzalishaji.

## Maswala ya kisiasa

Miundo ya utawala wa mji wa Dar es Salaam – yaani rasmi na isiyo rasmi – imegawanyika sana, ambapo inamaanisha kuwa juhudi za mageuzi/maboresho ya jiji zima zinahitaji uratibu makini wa wadau mbalimbali na maslahi tofauti. Hali ya kisiasa ya jiji pia imekaa na kuegemea upande mmojana uliotawanyika, na kuzidisha changamoto ya uratibu zaidi. Tangu awamu ya sasa kuingia madarakani mwaka 2021, demokrasia baina ya vyama na ndani ya chama imeendelea kushika kasi.

Wakati uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu ukikaribia mwaka 2024 na 2025, huenda utawala wa kisiasa wa chama kinachoongoza ndani ya jiji ukakabiliwa na ushindani. Kwa kuzingatia changamoto zote za kisiasa na kiutawala jijini Dar, viongozi wake wanaweza kuwa wazi/kuwa na utayari wa kufanya mageuzi/maboresho kuongeza juhudi kuelekea uchaguzi ujao, ili kuwasaidia kubaki madarakani kupitia wapiga kura wa mijini. Hata hivyo, mafanikio ya mageuzi hayo yatatokana na uratibu mzuri wa mifumo ya kiutawala na kukubalika kwa viongozi mbalimbali wenye nguvu katika ngazi za jiji na kitaifa.

## Domain/Eneo

Kwa kila domain, timu yautafiti ya jiji la Dar es Salaam ya ACRC ilibainisha masuala muhimu au vipengele vinavyodhaniwa kuzuia ukuaji endelevu wa jiji na mabadiliko. Inachukuliwa kama matatizo magumu ya kipaumbele (PCPs), yamefupishwa hapa chini kuhusiana na eneo/domain maalum.

### > Nyumba/Makazi (housing)

Upatikanaji wa nyumba za bei nafuu, za kutosha, zenye ubora jijini Dar es Salaam ni changamoto kubwa kwa wakazi wa kipato cha chini. Huduma za msaada wa makazi kama vile ardhi inayohudumiwa (maeneo yenye huduma mbalimbali), fedha na vifaa vya ujenzi sio nafuu, hulazimisha wamiliki wa nyumba kujijengea makazi kwa kudunduliza katika makazi yasiyo rasmi. Zaidi ya asilimia 90 ya hizi nyumba hujengwa kwa kutumia akiba ya kaya, mara nyingi hupitisha kanuni za upangaji na ujenzi kwa lengo la kupunguza gharama. Wadau katika sekta ya nyumba ni pamoja na serikali, watu binafsi, mashirika ya nyumba na huduma, asasi za kiraia, taasisi za fedha na mashirika ya kimataifa. Shughuli za wadau hawa zimegawanyika.

### PCP ya Nyumba (housing)

Licha ya mipango mbalimbali ya kusaidia fedha za makazi, kama vile WAT-SACCOS[1], Shirika la Nyumba la Taifa na benki za biashara,uwezo wa kumudu nyumba za gharama nafuu ni changamoto kubwa kwa watafutaji wengi wa nyumba na wajenzi jijini Dar es Salaam. Mibadala iliyopo haijaratibiwa vizuri na hazijawagusa vya kutosha wato wenye kipato cha chini. Matokeo yake, kaya nyingi hupata nyumba kupitia ujenzi binafsi wa kudunduliza kipato kidogo kidogo, ambao unaweza kuchukua hadi miaka 15 na mara nyingi nyumba huwa haziishi. Pia kaya nyingi huchagua vifaa vyenye ubora wa chini na ardhi katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko kwa kuwa bei yake ni nafuu. Wakati wadau wa kufadhili maswalaya nyumba/makazi wakilalamika kuwa mwamko ni mdogo, wale wanaotafuta fedha pia wanalalamikia ugumu wa kuipata. **Kuna haja ya kuelewa vizuri ni nini kinachozuia upatikanaji wa fedha na kuongeza mibadala iliyopo ya fedha.**

1 Women's Advancement Trust Savings and Credit Cooperative Societies/Chama cha Ushirika cha Maendeleo ya Wanawake cha Akiba na Mikopo



## > Makazi yasiyo rasmi (informal settlements)

Zaidi ya 80% ya wakazi wa jiji wanaishi katika makazi yasiyo rasmi yaliyojaa watu. Makazi haya ni kitovu cha shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo zinasaidia wengi katika jiji lakini kuna changa moto ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya makazi ya kipato cha chini na utoaji wa miundombinu ya msingi, ikiwa ni pamojana usafi wa mazingira. Licha ya mipango na mipango ya sera ya kudhibiti makazi yasiyo rasmi, changamoto hizi zinaendelea na kusababisha kuendelea kupungua na kupanua hali ya kutokuwa na usawa wa katika jamii. Ukosefu wanjia thabiti za kushikisha jamii katika mipango ya matumizi ya ardhi hukwamisha mipango endelevu ya maendeleo ya ardhi. Urasimishaji wa ardhi unaepukwa na baadhi ya wakazi kutokana na taratibu ngumu zinazohusika na hofu ya kanuni za kodi baada ya urasimishaji. Kushindikana kwa udhibiti maendeleo ya ardhi katika makazi yaliyorasimishwa kunaathiri wakazi na kusababisha utitiri wa ukuaji wa makazi yasiyopimwa kupita kiasi na kuathiri makazi yenyewe.

### PCP ya makazi yasiyo rasmi (informal settlements)

Ukuaji wa kasi wa makazi yasiyo rasmi bado ni changamoto inayoongezeka. Makazi yasiyo rasmi kupita kiasi husababisha hali mbaya ya maisha na kazi, yenye sifa ya ukosefu wa ardhi kwa huduma za msingi za miundombinu, na kuchangia usafi duni unaowaweka wakazi kwenye milipuko ya magonjwa. **Ili kukabiliana na changamoto hii, tunasema kuwa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi inayoongozwa na jamii inahitajika ili kupata ardhi kwa ajili ya utoaji wa huduma za msingi, ikiwa ni pamoja na usafi wa mazingira.**

## > Mabadiliko ya kimuundo/mifumo (structural transformation)

Mabadiliko ya kimuundo ya Dar es Salaam yamekuwa polepole, huku nguvu kazi ikiondoka kwenye kilimo kwenda kwenye uzalishaji wa huduma zisizo na tija na sekta zisizo rasmi, kama vile biashara ndogondogo, hivyo kudhoofisha sekta ya viwanda. Upatikanaji mdogo wa fedha, Upokeaji mdogo wa teknolojia na vyanzo visivyo vya uhakika vya nishati huchangia kuongezeka kwa sekta isiyo rasmi. Taratibu za usajili zimezuia uwezo wa biashara ndogondogo kurasimishwa na kufanyika kisheria. Hatimaye, sekta isiyo rasmi na uzalishaji mdogo unaendelea kuongezeka, licha ya kuwepo kwa taasisi na vituo vilivyoanzishwa vinavyosaidia ukuaji wa biashara ndogondogo. Kwa kiasi kikubwa, kuiweka pamoja (centralisation) mifumo muhimu ya jiji na miundombinu katika kukuza uchumi haiwezi kufanyika ipasavyo.

### PCP ya mabadiliko ya kimuundo/mfumo (structural transformation)

Sekta ya ujenzi ambayo inafanya kazi kwa ufanisi ni muhimu kwa maendeleo endelevu. Mabadiliko ya kimuundo ni muhimu kwa sababu sekta nyingine, kama vile miundombinu ya kijamii, hutegemea. Licha ya umuhimu wake katika maendeleo ya kijamii na kimazingira, mchakato wa kutoa vibali vya ujenzi ni mgumu na umegubikwa na masuala mengi. Hii imedhoofisha hasa ukuaji wa uchumi wa jiji. **Kuna haja ya kuanzisha center au sehemu moja mtandaoni ili kuboresha uratibu na kuongeza ufanisi wa kupata vibali vinavyohusiana na ujenzi ni muhimu.**





## > Maendeleo ya kiuchumi katika jamii (kuanzia ujirani/kitongoji) na wilaya (neighbourhood)

Biashara ndogondogo zimeenea katika viunga vyote vya jiji la Dar es Salaam. Zaidi ya nusu ya kaya zinajihusisha na biashara ndogondogo, huku wanawake na vijana wakitawala ubia huu. Licha ya mipango ya kusaidia biashara ndogondogo kupitia vikundi rasmi na visivyo rasmi katika ngazi ya chini, ukuaji endelevu wa uchumi haujafikiwa. Kuenea kwa biashara ndogo ndogo kunahusiana na muenendo wa maendeleo na ueneaji wa miundombinu. Upatikanaji wa nafasi (space) katika maeneo yanayofaa, huduma za usafiri wa uhakika na fedha ni muhimu kwa ukuaji wa maendeleo endelevu. Uendelevu wa baadhi ya biashara zisizo rasmi haueleweki, unaamuliwa na vipaumbele vya serikali na umaarufu wa kisiasa, hasaule unaowalenga wachuuzi na waendesha pikipiki.

### PCP ya maendeleo ya kiuchumi katika jamii (kuanzia ujirani/mitaa) na wilaya (neighbourhood)

Wasafirishaji wa kibiashara wadogo, pikipiki za kibiashara (bodboda) na teksi ni wadau muhimu katika kuhamisha bidhaa na watu kwenye masoko na maeneo ya kazi ambayo hayahudumiwi na mitandao ya usafiri wa umma. Hata hivyo, wasafirishaji hao wanazidi kuwa tishio kwa ulinzi na usalama wa wasafiri, abiria na watumiaji wengine wa barabara. **Kuna haja ya kutoa mafunzo yaliyoratibiwa, utambuzi sahihi wa wasafirishaji na kanuni za usafiri ili kuikomboa sekta hii katika jiji.**

## Taarifa hii kwa ufupi

Taarifa hii kwa ufupi imeandaliwa na Timu ya Utafiti wa African Cities Research Consortium ya Dar-es-Salaam.

**Taarifa ya picha:**
1. Picha iliyopigwa angani ya eneo la jangwani - Moiz Husein / iStock; 2. Picha ya hali mbaya ya usafi wa mazingira - D Schäfer, SuSanA Secretariat / Flickr; 3. Dereva wa Bodaboda jijini Dar-es-Salaam - Augustusyne / Wikimedia Commons; 4. Picha iliyopigwa angani ya mazi jijini Dar-es-salaam - Moiz Husein / iStock.

UK International Development
Partnership | Progress | Prosperity

ACRC is funded by UK International Development. The views expressed here do not necessarily reflect the UK Government's official policies.

## Find out more

www.African-Cities.org

@AfricanCities_

bit.ly/ACRCnews

AfricanCities@manchester.ac.uk